Ukatili wa Dhambi, Na Adhabu Iliyogharimu Kuondoa Dhambi Maishani Mwetu

Asante, Ndugu Thom. Naomba ufungulie sauti yote ya chombo hicho kidogo ulicho nacho, tafadhali. Karibu nishindwe kufika hapa usiku wa leo. Nilishikwa na homa. Nami niliahidi kuwapo hapa. Ndipo nikasema, nikamwambia Ndugu Neville, amwite Ndugu Cox aje hapa na amwambie. Nikasema, "Mwambie Ndugu Neville aendelee na afanye ibada, maana mimi nimepwelewa sana na sauti. Hata ni vigumu kwangu kutoa sauti."

2 Naye akasema, akarudi na kusema, "Afadhali uje, Ndugu Bill. Ninaamini litakuwa ni jambo zuri." Kwa hiyo, daima ni—niko tayari kufanya jitihada ya namna fulani. Kama ninii . . . Kweli nimepwelewa sana na sauti siwezi kuwahubiria, ila ninaweza kuzungumza nanyi kwa muda kidogo tu, kwa msaada wa kidude hiki kidogo hapa. Mimi . . .

3 Kila wakati ninapokuja Indiana, hupwelewa na sauti. Sijui ni kwa nini, lakini mimi—mimi huninii, kila wakati, hushikwa na mafua. Mahali hapa tulipo pako bondeni sana. Ninapoingia hapa, na inaonekana tu kama kwamba siwezi kuliepa. Ninaomba, inaonekana kwamba inakuja hata hivyo. Lakini—lakini daima ninajaribu kufanya vizuri sana niwezavyo na cho chote kile nilicho nacho. Kwa hivyo ndivyo ambavyo daima nimejaribu kufanya, kilicho bora sana tuwezavyo. Hayo tu ndiyo Mungu anayoheshimu . . . anayotarajia, hasa, samahani; ndiyo yote anayotarajia.

4 Sasa ninatumaini ya kwamba—ya kwamba Bwana wetu atawabariki ninyi nyote na atawapa baraka kuu katika ibada hii nzima, Ijumaa hii, Jumamosi, na Jumapili. Ibada zitaendelea usiku wa leo, kesho usiku. Sivyo, Ndugu Neville? [Ndugu Neville anasema, "Ndiyo."—Mh.] Inaendelea tu moja kwa moja kesho usiku.

5 Sina budi kushuka kuja hapa, na kisha niondoke hapa na nienda kule na kuzungumza na kundi la wamishenari walioko Louisville. Nafikiri—nafikiri aidha ni mataifa kumi na saba ama ishirini na saba yaliyowakilishwa kwenye mkutano wa wamishenari. Walinitaka nichukue dakika chache kesho usiku huko. Jumapi- . . . Jumapili asubuni ndiyo ninii . . .

6 Kuna nini? [Mtu mmoja anasema, "Waweza kumwombea mtu huyu papa hapa sasa?"-Mh.] Mwekee mkono wako, ndugu.

7 Baba yetu wa Mbinguni, tunaomba kwa Jina la Mwanao mpendwa, Yesu, kwenye wakati huu tu, kwamba rehema Yako na iwe juu yetu usiku wa leo, katika kuponywa kwa ndugu yetu, mtu yule anayeketi pale ambaye anaonekana ni mgonjwa sana wakati huu. Ulisema, "Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana mpate kuponywa." Nami naomba pamoja na watu hawa usiku wa leo, katika Jina la Bwana Yesu, ya kwamba utamponya ndugu yetu wakati huu. Wakati ndugu yetu amesimama pale huku amemwekea mikono, ikiwakilisha mkono wa Bwana wetu Yesu, nasi pamoja tunachangia maombi yetu na kuyatuma Kwako, katika Jina la Kristo, ili ndugu yetu apate kupona upesi kutokana na ugonjwa huu alio nao. Amina.

8 Bwana akubariki, ndugu. Nyote mpeni hewa kidogo. Kwa namna fulani amesongwa pale kidogo. Mbona, acheni atoke nje. Kama ukitaka kutoka nje, bwana, mbona, nenda moja kwa moja uchukue kiti huko nyuma ya jengo pale, mahali unapoweza kupata hewa kidogo.

9 Sasa, Bwana Yesu anajua shida zetu zote. Yeye ndiye anayetubebea mizigo yetu.

10 Na sasa Jumapili asubuhi, mapema, thenashara, ibada ya mapambazuko. Ni wangapi wanaopenda ibada za mapambazuko kwenye Pasaka? Tunatarajia baraka kuu. Kwa hiyo basi, Bwana akipenda, nitafanya ibada za mapambazuko; ni kutoka thenashara hadi saa moja. Halafu mtarudi nyumbani kwenye kiamshakinywa chenu, kisha mrudi. Na kwenye saa tatu na nusu, ibada ya kawaida ya shule ya Jumapili, Ndugu Neville atakuwa hapa. Na mara baada ya ibada ya Jumapili, nitafanya ibada za ubatizo kwa wale watakaobatizwa, asubuhi ya Jumapili ya Pasaka.

11 Kama hujabatizwa kwa kuzamishwa, na unataka kufanya hivyo; nawe ni Mkristo, unaamini katika Uungu wa—wa Yesu Kristo kwamba ni Mwana wa Mungu; na unataka kuchukua mahali—mahali pako katika ushirika wetu, kubatizwa, tungefurahi kuwa nawe hapa asubuhi ya Pasaka, kama saa nne na nusu, kwa ajili ya kuzamishwa. Mje na nguo zenu. Endapo huna zo zote, bila shaka, mbona, hasa sana wanawake, wao wana nguo ndefu mle ndani, saizi mbalimbali kwa ajili ya akina mama. Sidhani kwa sasa wana za wanaume wote. Lakini sisi . . . tuna furaha sana kuwa pamoja nanyi hapa asubuhi ya Pasaka.

12 Halafu Jumapili alasiri kutakuwa na ibada ya mazishi, kutoka kwa mtu fulani anayeishi huko vijijini, ama mahali fulani kutoka hapa, aliyekuwa . . . Ninaamini aliongolewa hapa chini ya mahubiri ya Ndugu Neville hapa wakati fulani uliopita. Ninaamini jina hilo ni East, ama kitu kama hicho. Walinipigia simu kutoka kwenye chumba cha mazishi na kuniuliza kama

mimi pamoja na Ndugu Neville na baadhi yetu tungekuja na kuimba na kufanya ibada ya Jumapili alasiri, kwenye muda wa saa nane, huko kwenye Chumba cha Mazishi cha Mottaz.

13 Mimi simkumbuki mama huyo, East, Yast ama East. Wengi wenu wameona jambo hilo kwenye gazeti, nadhani, usiku wa leo. Na . . . [Dada mmoja anasema, “Ndugu Bill?”—Mh.] Ndiyo. [“Huyo alikuwa ni Edna Justice; alikuwa akija hapa mara nyingi.”] Edna Justice, huenda mnamjua. Yeye labda ni mwanamke kijana. Sivyo? Hiyo ni kweli, dada? [“Ishirini na tisa. En-he.”] Kijana mwanamke. Ninaamini wao . . . Mamaye alikuwa akinipigia na kusema ya kwamba anaacha watoto wadogo wawili ama watatu. Kweli inasikitisha.

14 Inaonyesha tu uovu wa—wa maisha haya yaliyo na mwisho, sivyo? Lakini katika . . . Kama yeye alikuwa katika Kristo Yesu, ana hali njema zaidi, usiku wa leo, kuliko mtu ye yote anayeketi kwenye jengo hili. Yeye alitembea tu kupitia katika bonde la uvuli wa mauti ambao binadamu wote hawana budi kupitia. Na siku moja mimi na wewe itatubidi kupitia njia hiyo, pia, ila haitatulazimu kuvuka Yordani peke yetu, kwa kuwa Yeye ni Mwokozi wetu. Kwa hiyo sisi—sisi . . .

15 Kama ukitaka kuja kwenye Chumba cha Mazishi cha Motazz, ambalo liko kwenye Barabara ya Maple, kati ya Walnut na . . . La, ninaamini ni Barabara ya Locust na Wall, mkono wa kulia unapoelekea magharibi. Ninii . . . Sijui mahali ninii yao . . . Namba yake ni ngapi? [Mtu fulani anasema, “221.”—Mh.] 221. Ni pale mahali ambapo kile Chumba cha Mazishi cha Scott na Combs kilikuwa, nilipokuwa kijana. Na hiyo ni Jumapili alasiri, na kwenye saa nane.

16 Halafu Jumapili jioni, ibada za kawaida za Pasaka hapa tena. Labda tutakuwa tukihubiri juu ya ma—mauti, kuzikwa, na kufufuka, Jumapili usiku. Nasi hatujui yale Bwana wetu atakayofanya kwa ajili ya juma lijalo, kama ibada hizo zitaendelea, ama ni jambo gani, kwa ajili ya juma lijalo. Tunatumaini ya kwamba nyote mtakuwa—mtakuwa hapa Jumapili, mnaoweza kuhudhuria.

17 Ninawatambua wengi wa wahubiri walio hapa. Mtu fulani aliniambia ya kwamba Bw. Fuller alikuwa hapa, aliyekuwa . . . ama kuja kwenye mikutano yetu. Je! mtu huyo yuko hapa? Ndugu Fuller, si wewe ndiwe uliyekuwa ukinichukua, kule New York, mahali hadi mahali, kwenda kwenye mkutano? Ninafurahi kukuona, Ndugu Fuller. Bwana akubariki.

18 Halafu nilimwona mhudumu mwingine kijana hapa ambaye—ambaye Ndugu Thom hakumjua. Hata sijui jina la mwisho la mvulana huyo, lakini ninajua wanamwita Junior kule nyuma. Jackson, Ndugu Jackson, Junior Jackson, inua tu mkono wako wa mwisho, Ndugu Jackson. Tunafurahi kuwa pamoja nanyi. Yeye ametoka huko karibu na Elizabeth, huko kwenye

kanisa la Kimethodisti, ambako nitafanya ibada hivi karibuni, Bwana akipenda, kabla hatujarudi kwenda nje.

19 Sasa ule wito mkuu wa kwenda India. Na kila kitu kinazidi kuwa kigumu na kigumu, kila siku. Niombeeni.

20 Sasa, usiku wa leo, hii ni Ijumaa Kuu. Ni usiku ambao kwamba sisi . . . Loo, nadhani, Yerusalemu, kwenye wakati huu, ni . . . jua limechomoza vizuri sana sasa, Jumamosi asubuhi. Lakini siku nzima, watu wamejikokota pole pole kupanda njia ile ile ya kale kule ambamo ule msalaba ulifuta alama za miguu zenye damu za mwenye kuubeba; machozi yakihuzunisha nafsi zao, wakilia. Makanisa mengi makubwa, na kadhalika, leo, yamesherehekea wakati huu wa kumbukumbu hii kubwa. Kama kulipata kuwa na wakati ambapo ulimwengu unapaswa kuwa unasherehekea, ni sasa, katika majira haya ya taabu.

21 Nami sijui kama dada yetu, akiona kinanda hiki kidogo cha kale hapa . . . Na—napenda kinanda. Kwa namna fulani mimi ni wa mtindo wa kale. Na sijui kama tunaweza kupata sauti yake:

> Yesu, unihifadhi.

22 Ni mmoja tu wa zile nyimbo nzuri za moyoni, za mtindo wa kale, tulizokuwa tunaimba zamani za kale. Na sasa kama sisi sote tungejiunga pamoja katika huo. Ninaupenda.

> Hapa msalabani,
> Wajiao Kalvari
> Waponywe damuni.

23 Ni wangapi wanajua aya yake, hata hivyo? Vema, jiungeni moja kwa moja nami sasa. Na sasa hebu na tushushe mapazia yanayotuzunguka, na tuweke nia zetu kwenye miaka elfu moja mia tisa iliyopita, alasiri ya leo. Ni Dhabihu ya jinsi gani! Ulimwengu haujapata kujua kitu kama hicho. Iliutikisa ulimwengu mzima! Na sasa je! hivi hamtaki kukaa karibu na mahali hapo, ambapo mko katika mahali pa ushirika na baraka pamoja Naye?

24 Hebu sote na tuuimbe sasa, kwa ile njia tu ya mtindo ule wa kale, sasa, msininii . . . jinsi tu—jinsi tu ungaliuimba kama ungalikuwa peke yako sasa. Vema. Ndugu Thom, nisaidie kuuongoza, utafanya hivyo? Sina sauti kubwa sasa. Halafu tena, vema. Vema. [Ndugu Robert Thom anasaidia katika kuimba *Karibu na Mslaba*.

> Yesu unihifadhi
> Hapa Msalabani;
> Wajiao Kalvari,
> Waponywe damuni.
>
> Msalaba, msalaba,
> Humu nina sifa;
> Hata nitapumzika,
> Mahali pa raha.

25 Wakati mkiinamisha vichwa vyenu, mkitaka, hebu na tuuvumishe tu pole pole sana sasa. [Ndugu Branham na kusanyiko wanaanza kuvumisha *Karibu na Msalaba*—Mh.]

Karibu na Msalaba,
Nimepatikana,
Na pendo na neema,
Nimezungukiwa.

26 [Ndugu Thom anaendelea kuimba polepole pambio hiyo tena, *Karibu na Msalaba*—Mh.]

27 Sijui kama mngetaka tu sasa hivi . . . Hakuna mtu aliyewafanyia jambo hilo. Sijui kama hamtaninii tu . . . hamngetaka kuyaweka wakfu maisha yenu kwa Kristo tena, na, "Bwana, unikumbuke. Ninapenda ninii Yako . . . kuchoka, mateso, kutokwa na damu, kunifia mimi. Mimi sistahili, lakini nitainua mkono wangu sasa, Bwana, Nawe utaniona. Ninataka maisha yangu yawekwe wakfu tena." Mungu awabariki. Mungu awabariki. Vema. "Ninataka kujiweka wakfu tena Kwako sasa, Bwana, katika usiku huu wa Ijumaa Kuu." Mungu awabariki.

28 Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utawabariki hawa walioinua mikono yao, na hao ambao hata hawakupata ujasiri wa kufanya jambo hilo. Tunaomba ya kwamba Yeye atoshelezaye yote, usiku huu, atambariki kila mmoja wao.

29 Tunawazia juu ya Kalvari, Mungu, Mwokozi wetu, alipolazwa katika aibu; akashushwa chini, akatolewa mikononi mwa tajiri aliyeuchukua mwili Wake, baada ya kumsihi Pilato; akauchukua na kumfunga Yeye katika kitani safi, apate kuuweka kaburini. Ee Mungu, ni hisia ya namna gani iliyokuwa juu ya maskini hao wanafunzi; ilionekana kana kwamba walikuwa wameshindwa wakati huo. Yeye yule waliyekuwa wamemtumainia sana, sasa alikuwa ameshaondoka, lakini si kwa muda mrefu. Dhabihu tu iliyokuwa ikitokwa na damu, hivyo tu. Siku moja, masaa machache baadaye, Yeye alifufuka na ndipo furaha ikaingia.

30 Tusaidie, usiku wa leo, Bwana, tukiwa katika msimu huu, na iwe juu yetu, ya kwamba tutaona mateso ambayo yaligharimu ukombozi wetu, huzuni iliyogharimu sisi tuwe na furaha. Na naomba nafsi zetu . . . Usiku wa leo, Bwana, jalia tujiweke wakfu Kwako, na nafsi zetu zihuzunike, zikiangalia huko ng'ambo na kuona jinsi, Ee Mungu, jinsi kifo hicho kinavyotisha. Jinsi dhambi ilivyo katili! Nami ninaomba, Baba, ya kwamba utatubariki pamoja sasa.

31 Pia nisaidie Mimi, Ee Mungu, kama mtumishi Wako aliyesimama hapa akiwa na sauti mbaya sana, na watoto Wako wakingojea kusikia kitu fulani kutoka kwenye Neno. Nisaidie, Bwana, na uvunje Neno la Uzima, bure, kwa kila mtu, tunapoyaweka wakfu tena maisha yetu na mioyo yetu. Machozi ya mioyo yetu yanatiririka, kwenye kilindi cha moyo

wetu, tunapowazia juu ya hiyo Dhabihu. Tusaidie sasa, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

32 Ninataka tu kusoma kidogo sasa kama mtanisikiliza kwa makini sana kwa muda kidogo, na mniombee. Katika Isaya, sura ya 53.

33 Labda sisi, leo, tumesikia matangazo ya redio, na kadhalika.

34 Nilifikiri tu juu ya Kristo leo. Sikuweza kujizuia kwenda mahali fulani na kupiga magoti tu. Nami ilinibidi tu kulia, nilipowazia juu ya... wakati mawazo yangu yaliporudi nyuma kuona yale yaliyotukia pale Kalvari.

35 Sikuweza kusikia vipindi vyo vyote vya redio, lakini labda walihubiri kutoka kwenye Injili. Na labda kesho usiku tutaliendea kutoka kwenye msimamo huo.

36 Lakini, usiku huu, hebu na turudi kwenye Agano la Kale. Ninataka kuzungumza juu ya: *Ukatili wa Dhambi, Na Adhabu Iliyogharimu Ku—Kuondoa Dhambi Maishani Mwetu*. Katika Isaya 53, nabii, aliyetiwa mafuta, miaka mia saba na ishirini kabla ya kuja kwa Bwana, alisema maneno haya.

> *Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta?...mkono wa BWANA amefunuliwa nani?*
>
> *Maana atakua mbele zake kama mche mwororo, na... mzizi katika nchi kavu; Yeye hana umbo wala uzuri; na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani.*
>
> *Alidharauliwa na kukataliwa na watu; mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, alidharauliwa, wala hatukumhesabu kuwa kitu.*
>
> *Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu;* amechukua hofu zetu*; lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, amepigwa na Mungu, na kuteswa.*
>
> *Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.*
>
> *Sisi sote kama kondoo tumepotea, kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote.*
>
> *Alionewa, na...kuteswa,...hakufunua kinywa chake: kama mwana kondoo a—alipelekwa machinjoni, na kama vile kondoo anyamazavyo mbele yao wakatao manyoya yake; naam, hakufunua kinywa chake.*
>
> *Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa:... maisha yake ni nani atakayeisimulia? maana amekatiliwa mbali na nchi ya walio hai; alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu.*

Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya, na pamoja na matajiri katika kufa kwake; ingawa hakutenda jeuri, wala hapakuwa na hila kinywani mwake.

Lakini BWANA aliridhika kumchubua; amemhuzunisha; wakati utakapofanya nafsi yake . . . ama *wakati* wewe. . .*na wewe utaona. . .nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi, ataona uzao wake, na ataishi siku nyingi, na mapenzi ya BWANA yatafanikiwa mkononi mwake.*

37 Kama ningaliliita fungu la Maandiko, usiku huu, ningechukua kifungu cha 6.

Sisi sote kama kondoo tumepotea;. . .na BWANA . . . kila mmoja amegeukia njia yake mwenyewe; na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote.

38 Ninataka kuzungumza kwa muda mfupi tu. Daima sisi hufurahi wakati inapofikia kuwa na furaha ya Bwana katikati yetu; na jinsi ninavyofurahi pamoja nanyi, sana. Lakini hivi uliwahi kutulia na kuwazia gharama yake? Uliwahi kutambua tu gharama iliyo nyuma yake; kwamba ilikuwa ni hukumu gani na adhabu ya dhambi ilikuwa ni nini? Jinsi ambavyo dhambi ni katili, wakati ilipomfanya Mwana wa Mungu kwenda kule Kalvari, na Mungu angempiga, na kugeuza uso Wake toka Kwake, na kumpiga, na—na yeye angeteswa. Angalia kwamba Yeye alikuwa ni Nani.

39 Sasa ninataka kuwachorea picha ndogo tu, tunapozungumza sasa. Hebu sote na tusafiri kidogo, usiku huu, kwenye chombo kidogo, na hebu. . .chombo kidogo cha anga, ama chombo hewani. Hebu na turudi nyuma miaka milioni mia moja kabla hapajakuwapo na ulimwengu, kabla hata hapajakuwapo na nyota wala cho chote kile, na kule huwezi kuona cho chote ila anga. Na anga lile lote lilikuwa ni Mungu. Hapo mwanzo alikuwa Mungu.

40 Na sasa tutaona kukiwako na Nuru ndogo nyeupe. Tutaiita, tuseme, Duara ya Nuru. Na hiyo ilikuwa ni Mwana wa Mungu, yule Logos aliyetoka kwa Mungu, hapo mwanzo.

41 Halafu basi hivyo ndivyo alivyokuwa amesimama pale; Naye, niani Mwake, alianza kuwazia jinsi ulimwengu utakavyokuwa, ndipo akachora picha hii yote niani Mwake. Kisha akasema, "Iwe nuru."

42 Ndipo atomi ikapasuka na kuanza kuvunjika-vunjika, kisha atomi ikalipuka, mlipuko wa kwanza wa atomi. Ndipo atomi hizo zikaanza kukusanyika mpaka zikawa lava, kama unyevu, cho chote kile, ikaanza kuvunjika, ndipo zile atomi zikapasuka. Na punde, pakatokea nyota, ama kipande cha ninii. . .kombora lililoruka na kupita hewani. Yeye alikuwa akiangalia kwa labda milioni kadha ya miaka, kisha akaisimamisha. Hakuwa na haraka. Alikuwa na wakati mwingi sana, milele. Yeye alikuwa

tangu mwanzo hata mwisho. Kwake hakukuwa na wakati. Ndipo lingine likaruka, Naye akalisimamisha upande *huu*.

43 Yeye anafanya nini? Anaandika Biblia Yake ya kwanza. Biblia ya kwanza iliyopata kuandikwa, iliandikwa angani, ile Zodiaka. Inaanza na bikira, hivyo ndivyo Yeye alivyokuja mara ya kwanza. Inaishia na Leo yule simba, kule Kuja mara ya pili. Naye anaandika Biblia Yake ya kwanza.

44 Biblia ya pili iliyoandikwa, iliandikwa na Henoko, na kuwekwa kwenye piramidi.

45 Biblia ya tatu iliyoandikwa, na ya mwisho, ni *hii*. [Ndugu Branham anaonyesha Biblia yake—Mh.]

46 Mungu daima hufanya mambo katika utatu. Mungu anakamilishwa katika utatu. Yeye ni mkamilifu. [Ndugu Branham anakohoa—Mh.] Samahani. Yeye ni mkamilifu katika Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Ni mkamilifu katika kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Yeye anakamilika katika utatu Wake.

47 Sisi ni mfano Wake, kwa hiyo tunakamilika katika utatu; nafsi, mwili, na roho. Na mwili wetu unatawaliwa na—na neva, na damu, na kwa chembechembe (mwili); utatu. Yote hukamilika katika utatu.

48 Ndipo Yeye akasema, akiisha kufanya hayo yote, kabla hajawahi kufanya jambo lingine lo lote . . .

49 Ninaweza kuona Duara hii ndogo ya Nuru ikienda juu—juu ya dunia hii, ambayo ilikuwa ni lava tu, ilivyoganda, ikining'inia kule juu kama siwa barafu kuu. Naye akaisogeza karibu na jua. Ndipo akaanza kuigeuza namna *hiyo*, kulizunguka jua. Ikaanza kuyeyuka, na ile mito mikubwa ya barafu ikatokea. Texas ilikuwa ikiumbwa, na zile nyanda kule; kama vile tunavyofundishwa jinsi zile siwa barafu zilivyoshuka kupitia kule, jinsi wanahistoria hodari sana wanavyoweza kuwazia. Ndipo ulimwengu mzima, baada ya kutelemka mpaka kwenye Ghuba ya Mexico, na kadhalika, ukaanza kudondosha maji. "Nayo nchi, ilikuwa ukiwa, tena utupu," sasa tuko katika Mwanzo 1, unaona. Sasa, basi, Mungu akasogeza na kutenganisha anga na maji. Ndipo akafanya nuru.

50 Ndipo akaumba viumbe Vyake vyote. Halafu, baada ya kuviumba, miti yote ikachipuka, na mimea, na kadhalika. Ni mpango unaopendeza jinsi gani aliokuwa nao. Aliupenda. Ulikuwa mzuri. Naye akaona kuwa hilo linapendeza.

51 Kwa hiyo Yeye asingeweza kuiacha tu katika hali hiyo; ilimbidi kuiacha na kitu fulani. Kwa hiyo akasema, "Na tu-" (wingi)"-mfanye mtu," wingi, "katika mfano wetu." "Na tufanye mtu kwa mfano wetu wenyewe." Kwa hiyo basi Mungu alipomfanya mtu wake wa kwanza, Yeye alikuwa roho tu. Alikuwa ni kitu kama Mungu, ama Mwana wa Mungu, ile Logos.

Huyo alikuwa ndiye mtu wa kwanza. Ndipo akampa mtu huyo mamlaka juu ya . . . kuiongoza jamii yote ya wanyama, kama vile tu Roho Mtakatifu anavyomwongoza mwamini siku hizi. "Nenda *hapa*. Fanya *hivi*."

52 Sasa, kama tungalikuwa wakamilifu katika kujisalimisha kwa Roho Mtakatifu, Mungu angetuongoza, kwa Roho Mtakatifu, kama tu vile Adamu alivyowaongoza wanyama wa siku hiyo.

53 Kwa hiyo Yeye—Yeye aliwafanya. Halafu, wakati alipowafanya, alianza kuelekea kwenye—kwenye wazo basi kwamba—kwamba alikuwa amemuumba mtu kutoka katika mavumbi ya dunia. Hapakuwapo na mtu wa kuilima ardhi, hapakuwqpo na mtu wa kufanya kazi, hakuna mtu mwenye mwili. Kwa hiyo akamfanya mtu kwa mavumbi ya nchi.

54 Sasa hapo ndipo ninafikiri ya kwamba mtu mwenye elimu ya mi—mimea, ama—ama sayansi na Ukristo, havihitilafiani. Kwa sababu, sayansi inasema, mwanadamu alitokana na maisha tofauti; nasi tunasema, unapomwangalia mtu hapa, yeye yuko katika mfano wa Mungu. Huu ni, haukuwa mfano wa Mungu, kwanza. Huu ni mfano wa jamii ya wanyama. Naye . . . Nao wanamageuko wanasisitiza ya kwamba sisi . . . Mimi siamini katika mlolongo wa mageuko jinsi wao wanavyoamini, vyote vikitoka kwenye chembechembe moja. Lakini ninaamini tunageuka, bila shaka, mageuzi ya mtu mmoja kutoka kwa mwingine. Lakini basi wakati Mungu alipofanya hivyo vyote, na akaninii . . . akamweka mtu katika . . .

55 Akamfanya kutoka katika mavumbi ya nchi, sasa, si katika sura Yake Mwenyewe. Yeye alikuwa tayari amemfanya mwanadamu. Ndipo akampulizia pumzi ya uhai, ndipo akawa nafsi hai. Kwa hiyo, nafsi ya mwanadamu ni tabia ya roho.

56 Sasa, wakati unapozaliwa mara ya pili, hupati roho mpya. Unapata tabia mpya ya hiyo. Ni roho yule yule, lakini tabia mpya yake. Ukiwachukua watu wawili, uwasimamishe pamoja, wote wawili wanafanana; na mmoja wao ni mwenye dhambi, na mmoja wao ni Mkristo. Mtu mmoja anasema, "Nina roho yule yule uliye naye wewe," unaona. Lakini mmoja wao ni tofauti, nafsi yake. Tabia yake ni tofauti. Amebadilishwa.

57 Kwa hiyo basi Yeye alimpulizia mtu huyu. Sasa, sijui ni vipi, jinsi alivyomfanya. A—alimweka katika hisi tano ili apate kuwasiliana na makao yake ya duniani, na aone, aonje, aguse, anuse, na asikie. Naye alimfanya kwa jinsi hiyo. Sasa, hisi hizo hazikuwa za kuwasiliana na Mungu.

58 Hisi yake ya kuwasiliana na Mungu ilikuwa ni roho yake, nafsi yake ilikuwa ni ya kuwasi- . . . "Nafsi itendayo dhambi, nafsi hiyo itakufa."

59 Sasa, ninatumia maneno mengi, kusema kitu, lakini ninatumaini mnalipata kila wazo lake mpate kuona kile kilichombidi Mungu kufanya pale Kalvari.

60 Sasa wakati mtu huyu, basi, wakati Yeye alipomweka katika hisi zake, hisi zake tano. Halafu basi, mtu huyo, alikuwa mpweke, kwa hiyo akamfanyia mke, msaidizi, akatoa ubavu kutoka mbavuni mwake na kumfanya mwanamke.

61 Mfano mzuri pale, yote katika mfano, wa Mungu akitoa kutoka ubavuni mwa Kristo, Bibi-arusi. Unaona? Mungu alifungua ubavuni mwa Adamu, akatoa ubavu; ambao, mwanamke ana ubavu mmoja zaidi ya mwanamume, katika umbo la mwi—mwili. Na sasa Mungu akafungua ubavuni mwa Kristo, katika ninii . . . pale Kalvari, ndipo akamtoa Bibi-arusi. Kanisa linakuja kupitia katika Damu ya Kristo, na kuingia katika Mwili wa Kristo.

62 Hivyo ndivyo—ndivyo tunavyoingia, wala si kwa kupitia katika njia nyingine yo yote. Haidhuru wewe ni mfuasi wa kanisa gani, wewe u mtu mzuri jinsi gani, jinsi ulivyo mwanamke mzuri; huna budi kukubali Dhabihu ya Mungu inayotosheleza kwa vyote, njia Yake aliyoiandaa, la sivyo umepotea. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo tu unavyoweza kuingia, ni kwa kupitia Hapo. Sasa, kuna njia moja pekee, na hiyo ni ule Mlango.

63 Yesu alifundisha ule mfano maarufu, alipokuwa hapa duniani. Alisema karamu ya arusi ilikuwa tayari na—na kila mtu alipewa va—vazi, ndipo akamwona mtu mmoja mle asiyekuwa na vazi. Akasema, "Rafiki, je! unafanya . . . Vipi—vipi huna vazi?"

64 Sasa, mila za kimashariki za jambo hilo, hapo bwana arusi alipomwalika kila mtu, aliweka . . . aliowaalika. Kama alialika watu hamsini, basi alikuwa na majoho hamsini. Na alisimama mahali fulani mlangoni, na kila wakati mtu alipoingia, tajiri au maskini, alimvika joho. Ndipo, hakuna mtu aliyejua kama walikuwa matajiri ama maskini. Yeye, wote, walionekana sawa, katika vazi.

65 Na hivyo ndivyo Mungu anavyofanya siku hizi. Yeye humtoa Roho Mtakatifu; ambaye ni mfano. Kila mtu ambaye Yeye anaalika, sisi sote tuko sawa. Si ati *huyu* sababu ni bora kidogo kuliko yule mwingine, na *yule* ni mkubwa kidogo kuliko huyu. Sisi sote ni sawa machoni pa Mungu, kila mtu aliyealikwa kwenye Karamu ya Arusi.

66 Ndipo wakati alipoingia na kumwona mtu mmoja sasa . . . Sasa, kuna mlango mmoja tu wa kupitia, kwa maana huko ndiko mavazi yalikotolewa. Ndipo akamwona mtu kwenye meza ya karamu, asiye na vazi. Akasema, "Rafiki, unafanya nini hapa? Mbona huna vazi?" Ndipo mtu huyo hakuwa na neno la kusema. Alipitia dirishani, njia nyingine. Hakupitia mlangoni.

67 Na kila mtu anayekuja kwa njia ya Kristo, akaingia katika Mwili wa Kristo, hupokea Roho Mtakatifu, lile joho. Yeye

anasimama pale pale, kukuvalisha Hilo, mara tu unapoingia, unaona. Hivyo ndivyo alivyoahidi na hivyo ndivyo anavyofanya.

68 Sasa, nyuma huko katika ninii—hapo mwanzo, kule Edeni, basi Yeye alimfanyia mke, ama msaidizi.

69 Sasa unaona picha hizi katika magazeti, mara nyingine, za wanasanaa. Sasa, huo ni uvuvio duni sana. Kama ungalimwona Hawa na nywele zilizotokeza namna *hiyo*, na, lo, ni kitu cha kuchukiza namna gani, na kusema, "Huyo alikuwa ndiye mama yetu," mbona, hakungekuwa na mtu ulimwenguni angaliweza kupendezewa na kitu hicho. Ninaamini Hawa alikuwa mwanamke mzuri sana aliyewahi kuwapo duniani. Hiyo ni kweli. Wakati Adamu alipomwangalia, ninii yake, yeye—yeye . . . Ni kwamba tu, mbona, inaonyesha asili hiyo inakuja moja kwa moja kupitia kwa wanadamu leo. Kama haikupitia, ingekuwa vinginevyo.

70 Kwa hiyo, Adamu alimchukua Hawa kama mkewe. Ndipo basi wakati dhambi ilipoingia . . . Nami nina wazo langu kwamba hiyo ilikuwa ni nini. Silitamki huko kanisani, isipokuwa niwe na darasa dogo la aina fulani, kwamba ile dhambi ilikuwa ni nini hapo mwanzo. Lakini, hata hivyo, wakati ilipotokea, iliwatenga na ushirika wa Mungu.

71 Sasa hii hapa picha ninayotaka kupata. Sasa wakati Mungu alipotambua, ama Malaika fulani ama Kiumbe fulani kilipokuwa kimekuja na kumwambia Mungu, ya kwamba, "Mwanao amepotea. Yeye, yeye amefanya dhambi. Ameanguka."

72 Sasa angalia asili ya mwanadamu, jambo la kwanza, ni kujifanyia dini. Mwanadamu, ana namna fulani ya dini.

73 Nilikuwa nikizungumza na mtu mmoja maarufu hapa mjini, hivi majuzi. Kasema, "Unajua, dini yangu, Ndugu Branham, ni ya kushika Kanuni ya Msingi." Hilo ni jema.

74 Lakini, ndugu, mtu asipozaliwa mara ya pili, ataangamia. Naam. Hana budi kuzaliwa, hana budi kuzaliwa mara ya pili. Sasa, Kanuni ya Msingi ni sawa; hilo, mtu mwadilifu anaweza kufanya jambo hilo. Lakini jambo zima halina budi kufuata njia ya rohoni. Nawe utaona kile kilichombidi Mungu kufanya tupate kuzaliwa kiroho.

75 Sasa wakati, basi, wao walipofanya dhambi, a—alijifanyia di- . . . Neno *dini* linamaanisha "kifuniko." Ni kama kitu kinachofunika. Koti hili ni ninii—ni—ni dini ya uadilifu kwangu, kwa maana inafunika utu wangu. Na nguo zako ni kitu kile kile. Na ni ninii . . . Ni ki—kifuniko.

76 Sasa angalia basi, wakati, Adamu, majani yake ya mtini yalikuwa sawa mradi tu haikumlazimu kukutana na Mungu. Lakini ilipombidi kukutana na Mungu, alitambua ya kwamba majani yake ya mtini hayafai kitu. Na sasa, ewe rafiki, huenda

ukadhani wewe ni mtu mwema sana, unaona, na huenda ukawa mzuri. Hiyo ni kweli. Lakini utakapokuja kukutana na Mungu, ninii yako . . . kama hujaikubali Dhabihu iliyotolewa na Mungu kwa ajili yako, umepotea na utajua jambo hilo.

77 Nimesimama karibu nao, nikaangalia wakifa; nikaona daktari akiwadunga sindano mikononi mwao, kuwatuliza. Na kuwasikia wakilia na kupiga makelele. Waseme, "Loo, wamerukwa na akili tu."

78 Nikasema, "Dakta, naomba uiondoe, kwa dakika moja zaidi." Unaona? Nawe unaweza kuwasikia wakati wao—wao wanapofikiri wewe uko sawa.

79 "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti."

80 Na kila mtu asiyezaliwa mara ya pili, asiyezaliwa mara ya pili na Mungu, ataendea njia hiyo ya uharibifu. Huwezi kujizuia. Nafsi yako mwenyewe inakuongoza. Kama umezaliwa mara ya pili, huna budi kwenda juu. Kama hujazaliwa mara ya pili, huna budi kushuka. Ninii yako tu—nafsi yako mwenyewe itafanya jambo hilo. Ni kama ninii tu—kama tu fimbo ya kichawi ambayo ingefungua mlango mahali fulani; kama huna ninii hiyo—hiyo fimbo, mlango hautafunguka. Na kama hujazaliwa mara ya pili, unakataliwa tu, moja kwa moja. Hivyo tu, sasa.

81 Halafu wakati mimi ni—nionapo pale, basi, wakati wanapotoka nje, naye Mungu alijua ya kwamba hawangeweza kusimama mbele Zake. Na Yeye alijua. Nao walikuwa wakijificha, wakijificha nyuma ya vichaka fulani. Hata hivyo, wamejifunika, lakini walijua kujifunika kwao hakukutosha.

82 Na kila mwanamume ama mwanamke anayeenda kanisani . . . Leo nilikuwa nikifikiri juu ya makanisa makubwa yakipiga kengele, na kengele zikilia, na kadhalika namna hiyo; na watu wakienda kanisani, na kujitayarisha, na wanawake wakinunua kofia zao za Pasaka, na kadhalika. Jambo hili limefikia wapi? Jamani! Jinsi nisivyoweza kufahamu ambapo sungura ana uhusiano wo wote na ufufuo, unaona, (la, bwana) jinsi mti wa Krismasi ulivyo na uhusiano wo wote na Kristo. Ni upagani, rafiki zangu. Tumeacha njia mahali fulani. Hiyo ni kweli. Lakini sasa mwanamume aliyezaliwa mara ya pili ama mwanamke anatambua, kwa maana kuna uhai ndani yako, unaokwambia ya kwamba jambo hilo ni kosa. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

83 Sasa angalia; Adamu na Hawa. Loo, jamani! Ninapowazia jambo hilo, ninasahau flu yangu, cho chote nilichokuwa nacho. Ninapowazia, huko nyuma kabisa hapo mwanzo. Angalia! Unanena juu ya damu?

84 Hapa si muda mrefu uliopita, wakati walipokuwa wakiwazia sasa, katika lile baraza kuu la Kimethodisti, juu ya kutoa nyimbo zote za Damu kutoka kwenye kitabu cha nyimbo za

Kimethodisti. Kasema, "Si dini ya machinjioni." Kasema, "Sisi hatuninii . . . Tunataka kitu kizuri na cha kiungwana." Ndugu, hivyo sivyo Mungu alivyoipokea. Ni aidha . . .

85 "Nitakapoiona damu, nitapita juu yenu." Damu! Mungu, kitu pekee cha kibadala kilichoko, kiko tu katika . . . "Uhai umo katika damu. Mnaweza kula nyama zake, lakini damu yake, ambayo ndio uhai wake, imwageni ardhini." Mnaona, msile uhai.

86 Angalia jinsi lilivyo zuri! Jinsi ninavyowazia jambo hilo! Ndipo Mungu akawazia, "Sasa njoni huku, Adamu na Hawa. Na kabla sijawatoa nje, itanibidi kufanya jambo fulani." Kwa hiyo Yeye anaondoka anaenda kule kando ya kilima na kumchukua kondoo; anamuua, anachuna ngozi yake, anamwacha afe.

87 Kwa sababu, Mungu hana budi kudumisha Neno Lake, haidhuru wewe ni mtu mzuri namna gani, wewe ni mwanamke mzuri namna gani, cho chote ulicho. Ni, Mungu, Mungu hana budi kutimiza Neno Lake.

88 Hiyo ndiyo sababu ilimbidi bikira Mariamu kupanda juu, Siku ya Pentekoste, na kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, kama tu hao wengine walivyofanya, kwa maana alizaliwa hapa kama mwanadamu na ilimbidi kuzaliwa mara ya pili kabla hajaenda Mbinguni. Amina.

89 Sasa angalia, ewe bibi, hebu nikwambie. Kwa sababu tu eti nyakati zimebadilika, Mungu hajabadilika. Ukipungukiwa na jambo hilo kwa cho chote, umepotea. Unaona? Sasa, ninanena tu kwa niaba ya yale Mungu aliyofanya miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, leo, pale Kalvari, kukuonyesha ni Dhabihu ya namna gani iliyopaswa kufanywa kulipia jambo hili, na hiyo ni njia ya Mungu. Sasa iko njia inayoonekana sawa; lakini Mungu ana njia aliyoiandaa. Kama daima utapitia katika njia iliyoandaliwa na Mungu, hutakosea kamwe.

90 Ni kama vile ungeanza kwenda Indianapolis, ama kuvuka daraja, na unasema, "Vema, hapa, huu hapa ni Louisville?" "Naam." Na uende moja kwa moja *hivi*; utakwama haraka sana. Hiyo ni kweli. Ni vyema uchukue mchoro, ramani, na kuisoma uone unaelekea njia gani.

91 Na, kisha, *Hii* hapa ramani ya Mungu ya kwenda Utukufuni. Isome vizuri. Hiyo hapo. Imenyunyiziwa Damu kote njiani. Huwezi kupotea njia, endapo utaifuata ile Damu. Amina! Sasa unaweza kuona. Unaona? Ifuate tu Damu na utakuwa sawa, kwa maana kuna alama ya wayo wenye damu kwenye kila hatua ya njia.

92 Sasa angalia jinsi Mungu kule nyuma, kabla Yeye hajaweza kufanya jambo hilo, sasa angeweza kusimama ama . . . Hata kabla hawajaweza kusimama kupokea, Yeye angewaua sasa hivi. Ilimbidi kufanya hivyo, kwa sababu Yeye ni mwenye enzi. Hana

budi kutimiza Neno Lake. Yeye alisema, "Siku utakayokula, siku hiyo utakufa." Hilo lilitatua jambo hilo milele.

Ndipo ninaweza kumwona kule nyuma, wakati alipowaua kondoo hawa. Unasema, "Je! hao walikuwa ni kondoo, Ndugu Branham?" Ninaamini hivyo. Yeye alikuwa ni Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu.

93 Na ilikuwa ni ngozi ya kondoo; akaichukua na kuwatupia kule nyuma kwenye vichaka, na kuwaambia "Vaeni hizi, kisha mtoke, na kupokea."

94 Nami ninaweza kuwaona Adamu na Hawa wakijifunika hizi ngozi za kale zenye damu, zinazoning'inia. Ungeweza kuwazia? Miili mizuri, ya kupendeza, ya hao wanadamu wawili wakamilifu, sasa imevalishwa ngozi yenye damu. Ninaweza kuwaona wamesimama kule nje.

95 Mungu akasema, "Adamu, kwa sababu umemsikiliza mke wako badala ya Mimi, basi, nilikutoa katika mavumbi, na mavumbini utarudi."

96 Na, "Hawa, kwa sababu umemsikiliza nyo—nyoka badala ya Mimi, mbona, umeleta uhai . . . umeondoa uhai ulimwenguni, itakubidi kuleta uhai ulimwenguni. Nitazidisha huzuni yako, na tamaa yako itakuwa kwa mumeo," na kadhalika.

97 Naye akasema basi, "Nyoka, kwa sababu umefanya jambo hili, akaenda . . . " Yeye hakuwa ni mnyama atambaaye. Alikuwa ni mnyama, aliyetembea wima, mwerevu kuliko hayawani wote wa kondeni. Nishuhudieni, hayo ni Maandiko. Alitembea, kama mtu, na alikuwa amemdanganya. Ndipo akasema, "Na kwa maana ulifanya jambo hili, miguu yako inatoka, na utatembea kwa tumbo lako, siku zote za maisha yako. Na mavumbi yatakuwa chakula chako."

98 Nao hao papo hapo; hukumu. Ilimbidi Mungu kutimiza hukumu Yake, maana alikuwa ameinena. Naye ni Mungu; Yeye hawezi kuighairi. Hana budi kudumu . . . Kusudi awe Mungu, Mungu hana budi kutimiza Neno Lake. Hiyo ni kweli.

99 Kwa hiyo hapo ninaweza kuwazia ninamwona maskini huyo Hawa, wakati alipomwangalia Adamu, nywele zake ndefu za kimanjano zikining'inia mgongoni mwake. Macho hayo makubwa, maangavu, ya bluu yaliyoonekana kama anga, mahali Mungu alipoyafanya, majonzi yakitiririka; yakichanganyikana na damu iliyokuwa kwenye nguo, na zikining'inia mwilini mwake, Hawa. Adamu, na mwili wake wenye nguvu, akamshika na kumwegemesha kifuani mwake, na pale majonzi, yakichanganyikana, yakianguka, huku yakitiririkia kwenye ngozi za kondoo, damu ikitiririka. Damu, kila mahali. Hapo!

Sasa Yeye anasema, "Hamna budi kuondoka katika Uwepo Wangu."

100 Nami ninaweza kumwona Hawa na Adamu, huku wamekumbatiana, wakienda, wakiondoka namna *hii*, hizo ngozi za kale za kondoo zikipigapiga mguuni mwao, zimetapakaa damu, zikijipigapiga kwenye mguu wao. [Ndugu Branham alipiga makofi mara moja—Mh.]

101 Ndipo ninaweza kuona lile anga lote, ambalo lilikuwa ni Mungu. Mungu hakuwa na mwazo wa siku, wala mwisho wa miaka. Yeye ni wa milele na milele. Ninaweza kuona anga lote hilo likianza kusogea namna *hii*, likifikia kwenye umbo la faneli namna hiyo, nalo likashuka chini moja kwa moja, hapo alipoanza kuwaangalia hao maskini watu wawili waliokuwa wakishuka wakitoka kwenye bustani ya Edeni, ngozi za kondoo zilizojaa damu zikipigapiga mguuni mwao. Yeye hangeweza kuvumilia jambo hilo. Ndipo likashuka, loo, likashuka chini mpaka kwenye kiini cha moyo wa Mungu, kinachoendelezwa u-p-e-n-d-o, "Mungu alipenda sana . . . " Yeye kamwe hangalivumilia kuwaona wakiondoka.

102 Akawaita warudi, akasema, "Nitaweka uadui kati ya Uzao wako na uzao wa Shetani." Basi wakati jambo hilo lilipotendeka, ilikuwa pale Kalvari; wakati Mungu Mwenyewe aliposhuka kupitia kwa mwanamke, akizaliwa na bikira.

103 Jinsi ningetaka kuzungumzia hilo kidogo tu, huko Edeni. Angalia wakati walipofukuzwa Edeni kwa sababu ya uovu. Baraka zote zikakatwa kwa sababu ya uovu.

104 Nami nafikiri, usiku wa leo, hiyo ndiyo shida ya Kanisa. Baraka zote zinakatwa kwa sababu ya uovu. Haya basi.

105 Wamefukuzwa kutoka bustani ya Edeni! Sasa nawatakeni mwangalie, huyu hapa anakuja . . . wakati Kaini na Habili, hao wana wawili wa Adamu na Hawa, walipokuja kutoa dhabihu.

106 Ninaamini yule Kerubi mkuu alikuwa upande wa mashariki wa lango, na Upanga huo ukizunguka huku na huko, ukilinda lile lango pale la kuingilia Edeni. Angalia, Moto, Moto wa Roho Mtakatifu ukilinda lile lango.

107 Na, leo, huo ndio unaolinda lile lango. Kama unaogopa Roho Mtakatifu na Moto, hutaingia kamwe. Upanga wa Mungu, unaowaka moto! Mungu ni Moto ulao, akiulinda ule Mti, akiulinda ule Mti wa Uzima.

108 Na sasa angalia, basi, hii ni picha nzuri. Loo, jamani! Ninaweza kumwona Adamu ama . . . Kaini na Habili, hasa, wakifanya kazi sasa, ama wakitoka kwenda kutoa dhabihu. Ninaamini walijenga madhabahu yao pale pale kwenye lango, kwenye Kiti cha Enzi, mahali ambapo wangeweza kuabudia.

109 Angalia, huyu hapa Kaini anakuja. Labda alifanya kazi mwaka mzima, kazi ngumu, akifanya kila kitu alichoweza ili kupata matofaa yaliyo makubwa kuliko yote, ama maboga makubwa kuliko yote, ama cho chote alichokuwa nacho,

akavileta langoni. Akajenga madhabahu pale pale karibu na lango, katika Uwepo wa Mungu. Akaweka matunda yake yote, na zile yungiyungi kubwa na kila kitu, na akaviweka madhabahuni vizuri, kisha akapiga magoti na kumwabudu Mungu.

110 Sasa nawatakeni . . . Natumaini hili linaingia ndani kabisa, kuliko lilivyowahi hapo nyuma, mpaka mlipate, mnaona. Sasa angalia.

111 Kama Mungu alikutaka wewe uende tu kanisani, Kaini alikuwa na haki kama tu Habili alivyokuwa nayo. Kaini alimjengea Bwana madhabahu. Unasema, "Vema, Ndugu Branham, mimi sifanyi jambo hilo tu, bali ninatoa dhabihu. Ninachangia misheni za ng'ambo, na nina ninii . . . " Mambo hayo ni sawa. Mambo hayo ni sawa. Lakini Mungu anahitaji zaidi.

112 Kaini alifanya jambo hilo, mwenyewe. Unaona? Alileta dhabihu. Alimwabudu Bwana. Alipiga magoti na kumsifu Bwana, na kusema, "Bwana, mimi hapa. Mimi hapa, na nimekuletea dhabihu. Nimejenga madhabahu." Amina.

113 Kwa kifupi, "Mimi ni mfuasi wa kanisa." Limekolea kabisa? Angalia. "Mimi ni mfuasi wa kanisa. Ninakuamini Wewe." Litaingia myoni kabisa sasa. Hebu na likolee vizuri. "Mimi ninamwamini Mungu. Nimejenga madhabahu. Nimeleta dhabihu. Nami hapa, Bwana. Ninakuabudu Wewe." Na Mungu akampa kisogo. Hakika.

114 "Na asubuhi ya pasaka," kama vile mchungaji wa jiji hili alivyosema, "unajua ninalofanya, ewe mhubiri, kwenye asubuhi ya Pasaka?"

Nikasema, "Unafanya nini?"

Kasema, "Ninawaambia watu wangu wote, ninawatakia 'Krismasi njema.'"

Kasema, "Kwa nini?"

Kasema, "Sitawaona tena mpaka Pasaka ijayo.'"

115 Kila mtu anajitokeza wakati wa Pasaka, hivyo tu, wananunua kofia mpya na nguo mpya. Na hilo lina uhusiano gani na Kristo? Loo! Na kutakuwa na mamilioni ya dola yatakayotumiwa mwaka huu, kesho, katika milki ya Kiprotestanti, kwa yungiyungi, yungiyungi kubwa mno na nzuri; kila mshiriki atakuja na kuyaweka madhabahuni. Mungu hajali yungiyungi madhabahuni. Anakutaka wewe madhabahuni. Si yungiyungi; si dhabihu yako. Wewe ndiwe unayepaswa kuwa madhabahuni. Tofauti yake ndiyo hiyo. Kuweka kile Mungu anachohitaji madhabahuni, ni wewe.

116 Sasa ninawatakeni mwone jinsi ambavyo, ile asili, huyo alikuwa ni Shetani katika Kaini. Na angalia ya kwamba ninii hasa . . .

117 Sasa hili linapaswa kuwafanya mjisikie vizuri sana, baadhi yenu ambao ni wasafiri na wapitaji. Na hatuna budi labda kusema, “Vema, laiti tungaliweza kufanya jambo *hili* kanisani mwetu, na *lile*.” Ridhika. Haleluya! Afadhali niabudie katika chumba kidogo cha kale mahali fulani kwenye vichochoro vya zamani za kale, na niwe na Mungu ndani yake, kuliko katika kanisa kubwa la jimbo lisilo na Mungu. Hiyo ni kweli. Hakika. Hapo! Yeye alikuwa maskini. Angalia. Ndipo akaleta dhabihu yake, Kaini akaleta, na kuiweka pale juu. Sasa, angalia, yeye alitokana na ukoo wa Shetani, kwa maana alitarajia Mungu aipokee, kwa sababu ilikuwa ni matunda yanayopendeza, jambo alilofanya, yeye mwenyewe.

118 Na watu wengi sana husema, “Vema, mimi ni mwanachama wa mashirika fulani mbalimbali. Na hu—huchangia Msalaba Mwekundu, na ninachangia mashirika ya kutoa misaada. Mimi huyapa msaada makanisa. Vipi kuhusu hilo, Ndugu Branham?” Hilo ni sawa.

119 Lakini, “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hataingia katika Ufalme kamwe.” Angalia jambo hilo.

120 Mambo hayo ya kutoa misaada ni mazuri, lakini ni nje ya . . . Hiyo bado siyo njia aliyoandaa Mungu. Kaini alikuja kwa njia yake mwenyewe. Na wengi, usiku wa leo wanakuja kwa kupitia njia zao wenyewe.

121 Hata huwezi kulijengea hoja. Mbona, hoja hata haziwezi . . . Hoja zako hazifai. Hustahili kulijengea Hilo hoja. Kama ungeweza kulihoji, haingekuwa ni imani tena. Huna budi kulitoa kwa imani.

122 Sasa, unasema, “Ndugu Branham, unamaanisha sina budi kwenda kule chini na—na kujazwa na Roho Mtakatifu na kuendelea namna hiyo kama hao wengine?” Kama unatarajia kuwa pamoja na hao wengine, unapaswa kujazwa. Hivyo tu. Naam, bwana. Hivyo tu. Unaweza kuchukua . . .

123 Namani alikuwa na jambo lile lile. Mungu alimwambia nabii huyo, “Mwambie, ‘Nenda ukajichovya mara saba.’”

124 Akasema, “Maji haya si ni masafi zaidi na mazuri zaidi?” Lakini ilikuwa ni yale maji ya Yordani; yanaonekana mabaya sana mara nyingine.

125 Lakini laiti kila mmoja hapa usiku wa leo angeangalia Kalvari, na kile ilichomgharimu Mungu, miaka elfu moja mia tisa iliyopita. Na ungeinua mkono wako, useme, “Nitashika njia na wachache wa Mungu waliodharauliwa”?

126 Unasema, “Sina budi kujiunga na jamaa hao ambao Ndugu Thom . . . ama baadhi yao wanawaita ‘watakatifu wanaojifingirisha’?”

127 Ndugu, nimezunguka ulimwengu, karibu mara tatu, wala sijamwona mtakatifu anayejifingirisha bado. La, bwana.

Nimeona utakatifu, lakini sio watakatifu wanaojifingirisha. Hilo ni jina ibilisi alilolibandika Kanisa. Mungu alisema, “Pasipo utakatifu, hakuna mtu atakayemwona Mungu.” Unaweza kujiridhisha, juu ya jambo hilo. Hiyo ndiyo njia ya Mungu.

128 Unasema, “Watu wanaopiga makelele na kupaza sauti na kuendelea?” Ndugu, hivyo ndivyo ilivyo. “Mbona,” unasema, “hilo, hilo linaonekana la wenda wazimu, kwangu mimi.”

129 Hiyo ndiyo sababu unapaswa kuzaliwa mara ya pili. Unapozaliwa mara ya pili, basi haitakuwa ni “wenda wazimu.” Utakuwa pamoja nasi. Wao walidhania vile vile ulivyodhania wewe, wakati mmoja. Hiyo ni kweli. Walidhania vile vile ulivyodhani, mpaka walipolipata Hilo, wao wenyewe. Ni badiliko, wongofu. *Kuongoka* maana yake ni “kubadilisha” cho chote. Na mtu asipojifia mwenyewe . . . na kusema, “Bwana, sijui kitu juu ya jambo hilo. Niingize tu ndani.” Amina. Ndipo Mungu atafanya jambo hilo. Unaona?

130 Sasa, Kaini alisema, “Nimeweka haya yote chini.” Mungu akaikataa. Aliifanya ya kupendeza sana.

131 Na labda unafikiri, “Vema, nitahudhuria ibada ya mapambazuko; sina budi kuwa na kofia mpya.”

132 Msichana mmoja siku moja alikuwa aimbe katika mkutano wangu. Naye akasema, “Ndugu Branham . . . ” Mama yake alikuwa anafulia kwenye pipa la kufulia, kujipatia riziki. Na Yeye ilimbidi aweke moja ya hivyo “vinyonga” nyweleni mwake, mwajua.

133 Ni kitu gani, rangi ya makucha? Ama mnakiitaje kitu hicho, cho chote kitu hicho kilicho kwenye nywele zake? Ninajua hilo ni kosa. Siwezi kamwe kukumbuka jina la kitu hicho. Sijui mengi juu yake. Toni? [Mtu fulani anasema, “La. Pam.”—Mh.] Pam, ndani yake, ilikuwa ni hicho.

134 Na ilimbidi kuwa na moja kwenye nywele zake kabla hajaimba kwenye kwaya. Na maskini mama yake akifua nguo kwenye pipa la kufulia, kujipatia riziki. Wakati alipoenda na kujitia pam, nami nikasema nisingemruhusu aimbe, maana hakustahili kuimba wakati alipozifanyia hivyo. Kweli!

135 Mungu na atusaidie kudumisha usafi wa mimbara, kwa vyo vyote. Hiyo ndiyo shida ya ulimwengu siku hizi, katika ninii yao . . . ? . . . Sikiliza, ndugu. Ninaamini katika tukio la mtindo wa kale, huko nyuma kabisa vichakani, mahali unapong’oa mizizi yote ya uchungu, na kutifua udongo, hiyo ni kweli, na kupanda mbegu.

Sasa, angalia sasa, Kaini, yeye aliwazia, “Ule urembo.”

136 Wao wanafikiria, “Vema, sasa, kanisa letu! Tutajenga kanisa jipya.” Hilo ni sawa. Kila kitu ni cha urembo, ni sawa, kama

ukimchukua Bwana Yesu pamoja nalo. Halafu kama ukimpata Yeye kwanza, atashughulikia mengine.

137 Mtu fulani alisema, "Ndugu Branham, unaamini msichana huyu anapaswa kuja madhabahuni, akiwa namna hii?"

138 Nikasema, "Ndugu, majira ya kuchipua yanakaribia. Miti yote hiyo ya mialoni huku nje, kila mmoja wao, una majani uliokuwa nayo mpukutisho uliopita. Lakini haitubidi kwenda kutoa yale majani, kusudi majani mapya yaje. Acha tu uhai mpya uje, ndipo jani la kale litapukutika." Hiyo ni kweli. Amina.

139 Sikilizeni. Hebu niseme jambo hili, pia. Kama jani la zamani lisipopukutika, inaonyesha Uhai mpya haujaja. Usinikasirikie sasa. Ninazungumza juu ya Yesu. Vema. Ndiyo hivyo. Vema.

140 Angalia kile ilichomgharimu Baba yetu wa Mbinguni. Angalia alichofanya sasa.

141 Na hapo akaja Kaini, naye akatoa dhabihu yake. Akaabudu. Akaenda kanisani. Yeye ni mzuri tu kama jamaa huyo mwingine.

142 Esau alikuwa vivyo hivyo. Esau, katika tabia yake, alikuwa ni mtu mzuri zaidi kuliko Yakobo, muungwana zaidi! Alimpenda baba yake; na mambo yale aliyofanya! Lakini Mungu alimchagua Yakobo.

143 Angalia sasa wakati Habili alipokuja kutoa dhabihu yake, vema, ilikuwa ni tofauti kabisa wakati Habili alipokuja. Huyu hapa Habili anakuja. Hakufanya kazi, hakujaribu kupata kanisa lililo kubwa zaidi ya yote yaliyoko mjini ahudhurie. Hakujaribu kupata kundi la watu lililo zuri kuliko yote apate kushirikiana nalo. Amina. Alichukua tu kitu alichokuwa nacho na akaja. Hivyo tu. Alikuwa mchunga kondoo. Kwa hiyo alinyosha mkono tu akamshika mwana-kondoo, na kumfunga . . . nadhani hawakuwa na kamba ya makonge yo yote siku hiyo, kwa hiyo hapana shaka alichukua mzabibu na kumfunga tu shingoni mwake.

144 Lakini ilinena juu ya nini? Walimwongoza wakampeleka Kalvari. Yeye alikuwa ni Mwana-Kondoo. Kasema, "Kwa nini Yeye alizaliwa katika zizi?" Vema, wana-kondoo hawazaliwi manyumbani. Wanazaliwa katika mazizi. Nao waliongozwa . . . waliongozwa machinjioni kama mwana-kondoo. Nao wakamwongoza, wakamwongoza hata Kalvari. Yeye alikuwa Mwana-Kondoo wa Mungu, amina, tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Ninapowazia jambo hilo, pale! Huyu hapa mwana-kondoo wa Habili anakuja. Huyu hapa Mwana-Kondoo wa Mungu anakuja.

145 Ninapowazia jambo hilo, moyo wangu unageuka na kugeuka tu. Ninapowazia, mimi, maskini mwenye dhambi, asiyestahili, asiyemcha Mungu, akifa bila Mungu, bila Kristo, ulimwenguni, bila tumaini! Na katika wakati unaofaa Kristo akafa mahali pangu, yule Mzuri, na akadharauliwa na kukataliwa, kusudi

nipate kukubalika machoni Pake. Mahali pangu! Loo! Mimi siwezi kustahimili tu jambo hilo. Siwezi tu kuwazia jinsi angefanya jambo hilo kwa ajili yangu. Mimi nilikuwa nani? Ndipo, unasema, "Je! Yeye alifanya jambo hilo kwa ajili yako?" Naam.

146 Roho Mtakatifu alikuja, akanitafuta, siku moja, na kusema, "Yeye alifanya jambo hilo kwa ajili yako," nami nikamwamini. Nilimwamini. Naam, bwana. Nilimkubali, na nikaona kwamba ni kweli. Haidhuru watu walisema walikuwa nini, "walikuwa washupavu wa dini," ama cho chote kile; nilimwamini Mungu. Nami . . . Naye alifanya vile tu alivyosema.

147 Ninaweza kumwona maskini Habili. Angalia sasa. Jamani! Ninaweza kumwona Habili akienda na kuchukua mzabibu huu mdogo, ananyosha mkono na kumchukua mwana-kondoo mdogo wa kiume, wa kwanza kutoka kwa maskini mama kondoo, akamfunga kwa mzabibu huu shingoni. Huyu hapa anakuja, akimkokota. Hakuna uzuri sana katika jambo hilo, sivyo? Akamkokota kwenda huko. Ndipo akampeleka kwenye mwamba mkubwa, uliokuwa kule mashariki mwishoni mwa lile lango. Sasa angalia.

148 Labda Kaini alikuwa amefanya kazi ngumu mwaka mzima, apate mazao mazuri sana angaliweza kutoa, alidhania angemfurahisha Mungu kwa jambo hilo.

149 Na watu wengi husema, "Mimi nitaacha kusema uongo. Nitaacha kuiba. Nitaacha kuvuta sigara. Nitageukia kwenye tabaka la watu walio bora zaidi. Nitaingia kwenye shirika fulani."

150 Jambo lenyewe ndilo hili! Mungu hajali juu ya wewe kugeuza ukurasa mpya. Anakutaka wewe umpe Kristo moyo wako, na umwache akushughulikie. Si yale unayoweza kufanya. Hatuokolewi kwa kazi bora, bali tunanunuliwa kwa rehema Zake. "Si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu." Kwa kuwa sisi ni wa—kwa kuwa sisi ni wa Mungu kwa sababu . . . Si kile nilicho mimi, si kile ninachofanya, mimi mwenyewe. Ni ambacho Kristo, katika Mungu, amenifanyia mimi na kukufanyia wewe.

151 Angalia, mfano mzuri. Huyu hapa anakuja, akimkokota masikini yule mwana-kondoo mdogo, akimkokota. Ninaweza kuwazia maskini jamaa huyo akianguka, labda alijua kilichomngojea, akikokota masikini miguu yake. Mfano mkamilifu wa Kristo akiukokota msalaba, Mwana-Kondoo wa Mungu akishuka kupitia Yerusalemu, akianguka, mnyonge.

152 Huyu hapa masikini jamaa huyo anakuja, akilia. Na wakati alipomweka kwenye lile jabali, akamlaza juu ya mwamba, akachukua kipande kikali cha jiwe . . . Sijui, nadhani hawakuwa na visu katika siku hizo. Akamlaza namna hiyo. Akamshika kwa nyuma ya kichwa chake, na kumvuta namna *hii,* akatwaa kis- . . .

ama lile jiwe gumu, na kuanza kukata masikini koo lake, na jiwe hilo likaanza kugonga-gonga shingo Yake. Juu ya mwamba huo akafa yule mwana-kondoo, akitokwa na damu, akilia, damu ikitiririka, masikini mishipa yake ya damu imekatwa, damu ikiruka kila mahali. Maskini sufu yake nyeupe ikalowa damu nyekundu. Mungu akaangalia chini kutoka Mbinguni, na kusema, "Ndivyo hivyo. Sasa umelipata. Hiyo ndiyo njia." Damu ikiruka kwa nguvu kutoka kwenye vena zake ndogo.

153 Ilikuwa ni kitu gani? Ilihusu Mwana wa Mungu, miaka elfu moja mia tisa na kitu iliyopita, alasiri ya leo. Aliongozwa kutoka gerezani. Akapelekwa kwenye kiti cha hukumu; na kutoka hapo, hadi kwenye ukumbi wa kupigiwa mijeledi; kutoka hapo, akapandishwa Golgotha, akajikokota akapanda kilima hicho. Simoni, Mkirene, akimsaidia kubeba msalaba. Na hapo, akafa, kwenye ule Mwamba wa Kale, Damu Yake ikiwa imemwagwa. Mwili Wake umeachwa uchi. Haleluya! Mabonge makubwa ya mate machafu ya askari wenye mzaha usoni Mwake. Pamoja na hayo akasema, "Kama Ufalme Wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, ningemwomba Baba Yangu, angenipa majeshi ya Malaika ambao wangekuja na kunipigania Mimi. Lakini Ufalme huu si Wangu.

154 "Bali Ufalme Wako na uje. Mapenzi Yako yatendeke." Na utafika hivi karibuni. "Ufalme Wako na uje. Mapenzi Yako na yatendeke." Loo, jamani!

155 Wakati Billy Sunday aliposema, wakati mmoja, ya kwamba, "Katika kila mti paliketi Malaika," aliyesema, "Hebu sogeza tu mkono wako na kuelekeza kindole chako, hivyo tu ndivyo inavyokubidi kufanya. Mambo tutayamaliza hapa chini." Jamani, hiyo si ni kweli!

156 Pembeni Kaiyafa aliangalia, na kusema, "Aliwaokoa wengine; Yeye Mwenyewe hawezi kujiokoa." Hiyo ilikuwa ni sifa kuu sana aliyopata kupewa. Kama angalijiokoa Mwenyewe, asingeweza kuwaokoa wengine. Kwa hiyo alitoa uhai Wake, apate kuwaokoa wengine. Haleluya! Amina.

157 "Sisi sote kama kondoo tulikuwa tumepotea; Mungu aliweka juu Yake maovu yetu sisi sote. Aliongozwa machinjioni kama kondoo; na kuongozwa kama kondoo, kimya, mbele yao wakatao manyoya yake, hakufungua kinywa chake. Hata hivyo alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake; na kwa kupigwa kwake sisi tumepona." Ungewezaje kukataa upendo huo usio na kifani? Kumwona anapokwenda akiyumbayumba akipanda kilima; masikini mwili mnyonge, usio na nguvu, umeinamishwa na mzigo huo!

158 Ninawazia juu ya mshairi alipoketi pale siku hiyo, na kuliona mara moja jambo hilo, naye akaandika.

Huku miamba ikipasuka na mbingu zikiwa giza,
Mwokozi Wangu aliinamisha kichwa Chake akafa;
Pazia lililokuwa wazi lilionyesha njia
Ya kufikia furaha za Mbinguni na siku isiyo na mwisho.

159 Ni Mwokozi wa ajabu jinsi gani! Loo, jamani! Tungewezaje kamwe, ningewezaje, kukataa upendo kama huo usio na kifani, kwa Mtu ambaye angefanya hivyo kwa ajili yangu na kwa ajili yako?

160 Ninatumaini, usiku wa leo, ndugu yangu, dada, ya kwamba utakuja. Mungu, hiyo ilikuwa ni njia iliyoandaliwa na Mungu. Hiyo ndiyo njia kwa ajili yako. Huyo ndiye tu anayeweza kukushughulikia. Huyo ndiye aliyepachukua mahali pako. Huyo ndiye anayesimama usiku wa leo, Mkombozi aliyefufuka, akisimama mkono wa kuume wa Baba, usiku wa leo; anakuona ukiomba na kusihi kwa ajili ya kila mwenye dhambi aliye kwenye jengo hili, kumjia Yeye. Ninatumaini ya kwamba utafanya jambo hilo. Ninatumaini ya kwamba hutaacha hii—hii Pasaka ipite.

161 Marafiki wapendwa, tumefikia mwisho wa barabara. Ninaamini tumefikia mwisho, kwa moyo wangu wote. Tumefika mwisho wa barabara. Bwana Yesu na awabariki. Na awafanye kiumbe kipya katika Yeye, usiku wa leo, ndio sala yangu. Na awaongoze. Wakati mmoja katika . . .

162 Kulikuwako na maskini kipofu katika Biblia, jina la—lake Batimayo. Maskini kipofu Batimayo, alikuwa na hua wawili wadogo, tunaambiwa na historia. Ya kwamba hawa hua wawili walitoka na kubingirishana, nao watu wange—wangeshika ninii zao . . . Yeye angeshika kikombe chake, halafu wakati wa—watu wangepita, karibu wangewaangalia maskini hua hawa wakijibingirisha, nao wangemtolea sarafu huyo maskini mwombaji kipofu. Alikuwa ameoa na alikuwa na msichana mdogo. Hajapata kumwona msichana huyo mdogo, maishani mwake. Yeye msichana alikuwa na umri wa miaka kumi na miwili hivi, miaka kumi na minne, katika kipindi ambacho tunataka kuingilia maisha ya babaye sasa. Naye alikuwa ameketi . . .

163 Usiku mmoja, inasemekana msichana wake mdogo aliugua, ndipo akamwendea Bwana. Pamoja na hayo akasema, "Bwana, kama tu utamponya maskini msichana wangu, nitakutolea dhabihu hua wangu wawili, kesho." Kwa hiyo wao . . . Bwana akamponya maskini msichana wake, naye akawatoa sadaka wale hua wawili. Na baada ya kitambo kidogo, ninii yake . . .

164 Na muda si muda unajua, mkewe mpendwa akaugua, naye alidhani ataninii . . . Walidhani atakufa. Ndipo akamwendea

Bwana, usiku, akipapasa-papasa ukuta wa nyumba yake. Akapiga magoti shambani, na akasema, “Mungu, Mungu, kama utayaokoa maisha ya mke wangu, kesho nitakutolea sadaka mwana-kondoo wangu.”

165 Sasa, mmewaona vipofu wakiongozwa na mbwa siku hizi. Wao wanawafunza mbwa hao kuwaongoza. Katika siku hizo, waliwafunza kondoo kuwaongoza watu, na kwa hiyo alikuwa na mwa—mwa—mwana-kondoo aliyemwongoza kila mahali.

166 Ndipo akasema, “Bwana, kama ukimponya tu mke wangu, vema, basi, kesho nitakutolea mwana-kondoo wangu sadaka.” Na mke wake akapona.

167 Basi kesho yake alikuwa akienda hekaluni, na ikasemekana kuhani mkuu, Kayafa, alisimama na kusema, “Kipofu Batimayo, unaenda wapi?”

168 Akasema, “Ninaenda hekaluni, Ee kuhani mkuu, kumtoa mwana-kondoo wangu dhabihu. Nilimwahidi Bwana, kama akimponya mke wangu, ningemtoa Mwana-Kondoo wangu.”

169 Akasema, “Huwezi kumtoa Mwana-Kondoo huyo, Batimayo, kwa sababu Mwana-Kondoo huyo ndiye macho yako.” Kasema, “Nitakupa pesa, nawe na ujinununulie Mwana-Kondoo kwa wauzaji humu hekaluni.”

170 Lakini Batimayo akasema, “Ee kuhani mkuu, mimi sikumwahidi Mungu Mwana-Kondoo ye yote yule; nilimwahidi Yeye Mwana-Kondoo *huyu*.” Loo, jamani!

171 Sijui kama umefanya ahadi kama hiyo. Kama ukimwona huyo Mwana-Kondoo anayetosheleza kwa vyote usiku wa leo, wazia. “Bwana, kama ukiniponya, ninakuahidi nitakutumikia Wewe; nitafanya yote niwezayo. Kama ukimjalia mtoto wangu mchanga kuishi . . . ” Ama, unaposimama na mama yako alikuwa akishuka kwenda kaburini, ama baba yako ama wapendwa wako, “Ee Mungu, nitakutana nao, nitakutana nao tena!” Sijui kama kweli ulimaanisha jambo hilo. Sijui kama Pasaka hii itakuja na kuondoka bila ya wewe kutimiza yale uliyoahidi.

172 Akaenda moja kwa moja na kutoa Mwana-Kondoo wake. Akarudi, mtu fulani akimwongoza kila mahali.

173 Kwa hiyo akasema basi, wakati aliporudi, kasema, “Batimayo, huwezi kufanya hivyo.” Kuhani yule aliyeenda kumchukua mwana-kondoo wake, akasema, “Huwezi kumchukua huyu. Huwezi kumtoa dhabihu mwana-kondoo huyu.” Kasema, “Kipofu Batimayo, je! unajua huyo Mwana-Kondoo ndiye macho yako?”

174 Akasema, “Naam, ninajua jambo hilo. Lakini nilimwahidi Mungu, naye Mungu ataitoa Mwana-Kondoo kwa ajili ya macho ya kipofu Batimayo.”

175 Haikuchukua muda baada ya hayo, alikuwa akitetemeka kwenye baridi, siku moja; wakasikia makelele. Mungu alikuwa

ameandaa Mwana-Kondoo kwa ajili ya macho ya kipofu Batimayo. Akaja barabarani. Akasema, "Kelele hii yote ni ya nini?" Kwa kawaida huwa kuna makelele po pote Yeye alipo. Kasema, "Kelele hizi zote ni za nini?"

Akasema, "Mtu mmoja, Yesu wa Nazareti, anapita."

176 Akatupa koti lake chini, bila kuangalia lilikoangukia; hakujali wakati huo. Mungu alikuwa amempa Mwana-Kondoo. Akaenda moja kwa moja kwa Mwana-Kondoo huyo. Akasema, "Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu! Unirehemu!"

177 Matajiri na hao waliosimama kando-kando, wapate kumkaribia nabii, yule mfalme; akasema, "Loo, tulia, Yeye hawezi kukusikia."

Akalia hata zaidi.

178 Baadhi yao walisema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama cha siku ile."

179 Akalia kwa sauti kuu zaidi, "Ewe mwana wa Daudi, unirehemu! Unirehemu." Mungu alimtoa Mwana-Kondoo.

180 Mwana-kondoo yuyo huyo Yeye aliyemtoa kwa ajili ya macho ya kipofu Batimayo, Yeye amemtoa kwa ajili yako; miaka elfu moja mia tisa na kitu iliyopita, leo, alipokuwa anakwea Golgotha, kule, na akajitoa Mwenyewe, amejeruhiwa sana na kukatwakatwa pamoja.

181 Sikiliza, ewe rafiki. Kumbuka, Habili alienda kwenye kundi lake na kumchukua mwana-kondoo, na kumwua madhabahuni. Na . . . [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] . . . afadhali ushike jambo hili sasa. Habili alikufa kwenye mwamba ule ule ambao mwana-kondoo wake aliofia.

182 Uko tayari, usiku wa leo, kujifia mwenyewe? Uko tayari kujifia kwa mawazo yako yote? Kaa tu kwenye mwamba, pamoja na Mwana-Kondoo wako pale, ufe. Sema, "Ee Mungu, unirehemu." Ninapofikiri juu ya wanaume na wanawake wanaowazia kiburi, vijana wanaume na wanawake watakaoyatoa maisha yao kwa ajili ya vitu! Na watu wazima, pia, wanaowazia juu ya kazi zao na sifa zao na ujirani wao, ama kitu kama hicho!

183 Loo, kwa nini usitambae kwenda kule Kalvari, usiku wa leo? Haleluya! Uache maisha yako mwenyewe yakatwekatwe, na yafie huko msalabani pamoja Naye. Ukumbatie ule "Mwamba wa Kale, uliopasuliwa kwa ajili yangu, hebu nijifiche Kwako. Wakati maji ya kale, yaliyo karibu yanapotiririka, wakati tufani ingali kubwa, nifiche, loo, Mwokozi wangu, nifiche. Acha ulimwengu ufanye lo lote utakalo. Acha wanatheolojia wafanye lo lote watakalo; mimi sitaki theolojia yao. Kile ninachotaka ni Yesu Kristo moyoni mwangu. Hebu nife pamoja na Mwana-Kondoo wangu."

184 Loo, ninajua jinsi lilivyokuwa jambo gumu usiku ule nilipotembea kuingia katika maskini ile misheni ndogo ya watu weusi sehemu zile, na wazungu wote wakiwa wamesimama kule kote, kasema, “Huyoo anaenda kwenye misheni ya watu weusi.” Lilikuwa ni jambo gumu. Nilienda kule nikiwa nimejaa kiburi chote cha Kentucky, namna hiyo, lakini Mungu akasema, “Kama unataka jambo Hilo, nenda moja kwa moja kule ndani.” Ndipo nikaingia moja kwa moja kule ndani na kupiga magoti madhabahuni, ndipo nikakaa pale mpaka Mwana-Kondoo . . . Nikajifia ule utu, Bill Branham, miaka ishirini iliyopita. Halleluya!

185 “Nilisulibiwa pamoja na Kristo. Hata hivyo mimi ni hai; si mimi, bali ni Kristo aishiye ndani yangu.” Siku moja katika ule ufufuo wenye utukufu, wakati atakapokuja, mwili wangu pengine unapumzika chini ya bumba la udongo na nyasi kule. Lakini muda utakapowadia, utaona nyasi zikiondoka nami nitafufuka, katika sura yake kuu yenye utukufu, pamoja na wengi wao, haleluya, kwa kuwa ninamjua katika Nguvu za kufufuka Kwake.

186 Ninatumaini hivyo ndivyo kila mmoja wenu atakavyofanya, usiku wa leo, kujikokota kupanda moja kwa moja mpaka huko Golgotha, usiku wa leo. Hebu na tufanye safari ndogo sasa.

187 Wakati, hebu tupe sauti, tafadhali, dada, ya *Karibu, na Wewe, Mungu Wangu*. Wakati tukininii . . .

188 Unasema, “Huo ni wa mazishi.” Vema, ndugu, kama paliwahi kuwapo na wakati tulipohitaji mazishi, ni sasa hivi, wakati watu watakapojifia wenyewe na kiburi.

189 Hebu tuinamishe vichwa vyetu, kwa kimya sasa, wakati anapotupa sauti ndogo, kama hiyo ni sawa.

190 Ee Mungu, loo, ninapofikiria kile kilichotendeka kule! Loo! Hata mifupa yangu inatetemeka, kuwazia! Ninawazia juu ya kumwona yule Mwana-Kondoo, wakati walipomkatakata, naam, wakamvika miiba kichwani Mwake na kuishindilia. Askari wakamtemea mate usoni Mwake, na kusema, “Ewe Mfalme, sasa fanya kitu kuhusu jambo hilo.”

191 Yeye alikuwa Nabii wa manabii. Waliweka tambara usoni Mwake, na wakampiga kichwani, kwa kizingiti, kasema, “Sasa tabiri, tuambie ni nani aliyekupiga.”

192 Lakini nabii akasema, “Hakufungua kinywa Chake.” Alikwisha nena jambo hilo.

193 Wakamfunga mikono Yake, nyuma Yake. Wakasimama kwa mbali, wakiwa na mjeledi mkubwa, na kumcharaza mpaka mbavu Zake za thamani zikatokeza mgongoni Mwake; Damu ikitiririka ubavuni Mwake, ikidondoka ardhini. Ninamsikia akitembea sasa; kutoka kwa ndara Zake ninasikia damu

ikidodoka. Huyo alikuwa ni Imanueli. Huyo alikuwa ni Mungu, Damu ya Mungu.

194 Nami niliwaona wakichukua, wakaweka huo msalaba mgongoni Mwake; ule msalaba wa kale wenye malengelenge, uliotatuka, unaoparuza. Pia Huyo hapo anaenda, msalaba umelala juu ya mgongo huo wenye majeraha, akapita barabarani. Umati uliokuwa ukipiga makelele, ukicheka, na ukimfanyia mzaha, "Huyo hapo yule Nabii anaenda. Huyo hapo yule Yesu anayesifiwa anaenda. Huyo kule Mponyaji wa Kiungu anaenda."

Lakini Yeye ni Bwana wangu! Ee Mungu, nimeninii . . . Hebu nipande pamoja na Yeye.

195 Huyo hapo anaenda, anapanda kilima. Ninaona vijana wanawake, nusu uchi, wakikimbia huku na huko, wakifanya mzaha. Marafiki zao wa kiume, wakikumbatiana, wakipanda kilima. Ndugu Ward, jambo hilo halijabadilika sana bado.

196 Ninaweza kuwaona wafuasi wakuu wa kanisa, wakisema, "Tazama, huyo ni yule Jamaa aliyekuwa anataka kulivunja kanisa letu; akahubiri kumpinga mchungaji wetu. Mwone sasa!" Lakini nabii alisema haina budi kuwa hivyo. Yeye alikuwa ni Mwana-Kondoo wa Mungu.

197 Ninamwona anapogeuza kichwa Chake, na mate yakiteleza kwenye ndevu Zake. Anainua macho Yake kuelekea Mbinguni; anaugua, na kwenda mbali kidogo.

198 Bwana, kwa imani, ninataka kuipita hiyo sasa pamoja Naye. Ninataka kumpigapiga mgongoni, niseme, "Bwana, nitasimama hapa. Niambie tu la kufanya, nitalifanya. Jinsi ninavyokupenda, Bwana!"

199 Huko mbali kilimani, walipomlaza chini, wakaivuta mikono Yake yenye thamani kubwa kwa nyuma. Mikono hiyo iliyokomesha homa; mikono hiyo iliyosema . . . na yule mvulana wa maskini mjane, wakati ilipogusa paji la uso wake, ama sanduku alimokuwa amelazwa; akafufufka.

200 Yule aliyemfufua Dorkasi. Yule aliyemfufua binti wa Yairo. Yule aliyesema, "Lazaro, njoo huku." Midomo hiyo inatokwa na damu sasa, inakauka kwa kiu, akilia.

201 Wakati ile misumari mikubwa na mikatili ilipokomelewa mikononi Mwake na miguuni Mwake! "Walinichoma mikono na miguu," alisema nabii, miaka mia saba kabla halijatendeka. Ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni Mwana-Kondoo wa Habili. Huko wakamtupa chini kwa nguvu, ndipo mwili ukachanika. Maskini mwili wake ukatetemeka.

Kasema, "Ninaona kiu." Wakampa siki.

202 Wakamkera na kumfanyia mzaha, na kumtania, wakasema, "Ewe mfanya miujiza mikuu, fanya kitu juu ya jambo hilo sasa."

203 Lakini basi mbingu zikaanza kuwa giza, umeme ukaanza kumulika. Mungu alikuwa akiuficha uso Wake; Yeye hangeweza kustahimili jambo hilo tena. Ee Mungu, jinsi dhambi ilivyo katili! Ni katili jinsi gani, ni katili jinsi gani, iliyosababisha huyo Mtu wa thamani kufanya hivyo. Hata gharama aliyolipa mpaka Mungu Mwenyewe akaficha uso Wake. Malaika walifunika nyuso zao na kugeuka kando, wakilia pamoja Naye. Mwezi na nyota hazingeenda mbali zaidi. Hazingeweza kuangaza tena. Mungu Mwenyewe aliyeziumba alikuwa anakufa msalabani. Naye akainamisha kichwa Chake.

204 Kabla Yeye hajafanya jambo hilo, aliangalia hao watu kule chini wakipigia kura vazi Lake, wakitimiza aliyosema nabii. Kasema, "Baba, wasamehe; hawajui watendalo." Wote wakiwa katika upendo, Mwana-Kondoo wa Adamu, Mwana-Kondoo aliyetolewa na Mungu, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Hapo akafa, bila rafiki, hata ameachwa na Mungu Mwenyewe. Mungu, na, basi, Baba Yake Mwenyewe, alimwacha; akitokwa na damu.

205 Hata hivyo, tunaenda huko na huko tukicheka, wenye furaha, kama tu kwamba hakuna jambo lililokuwa limetukia.

206 Ee Mungu, ilikuwa ni hiyo Damu! Wakati nikiwa niko kule hospitalini, daktari alisema "anakufa," hiyo Damu ilikuwa ndiyo iliyoniponya. Maskini mvulana mdogo mwenye dhambi akizurura hapa, hiyo Damu ndiyo iliyonisamehe dhambi zangu. Hiyo Damu ndiyo iliyochukua . . . iliyonitoa kutoka kwenye ufisadi nilimokuwa nikiishi, na kuniweka na kunifanya Mwanao. Loo . . . ? . . . na Mwana-Kondoo anayekufa, Damu Yako ya thamani! Niweke karibu na msalaba, Bwana.

207 Hilo ndilo ono langu. Hivyo ndivyo ilivyo kule ng'ambo, upendo, moyo wote mkuu wa Mungu ukifanya kazi pale. Na wote wamjiao Yeye hawatakataliwa. Wote watapokea Uzima wa milele. "Yeye anijiaye Mimi sitamtupa nje kamwe."

208 Mungu, jalia kila mtu hapa aende nyumbani, usiku wa leo, akiwa na hili niani mwake, akiwazia juu ya, "Ni Dhabihu ya ajabu jinsi gani! Iligharimu nini kukomboa? Ilimgharimu Mungu nini?" Haikutugharimu kitu. Ilimgharimu Mungu Mwanawe. Iligharimu Mungu gharama ya juu sana. Ilimgharimu Kristo maisha Yake. Yeye alikuwa ni Ua la Uwandani; lakini kupata manukato kutoka kwenye waridi, huna budi kuliponda-ponda. Uhai Wake mzuri ulipondwapondwa, akiwa kijana Mwanamume mwenye umri wa miaka thelathini na mitatu na nusu, kusudi tupate kuishi.

209 Karibu, na Wewe, Mungu wangu! Kaa karibu nami, Bwana. Kaa karibu nami. Na nitakapofikia mwisho wa safari hii, uhai wangu unaisha, Bwana; naomba Yeye, aliyekufa pale, anikaribie basi. Naomba kila mmoja aliye hapa ndani awe vivyo hivyo.

210 Kesho, Bwana, ama kesho kutwa, tutamzika maskini mwanamke mmoja aliyekuwa akiketi hapa katika kanisa hili wakati mmoja, akisikiliza mahubiri. Wewe unajua yote juu yake sasa. Kama yeye alikuja, yeye yuko salama. Kama hakuja, amepotea.

211 Ee Mungu, turehemu. Jalia kila mwanamume na mwanamke, wanapoondoka kwenye jengo hili usiku wa leo, waende manyumbani mwao; waende, wakiwazia kwa makini, "Sina cha mkononi; naja tu kwenye msalaba Wako." Na jalia kila mmoja wao afe kwenye msalaba huo.

212 Bwana, wakati niko hapa kwenye mimbara hii usiku wa leo, jengo hili dogo la kale la saruji, ninayaweka maisha yangu wakfu Kwako. Nakushukuru kwa yale uliyonitendea. Nami najiweka wakfu, katika usiku huu wa kusulubishwa kwa ukumbusho Wako. Nichukue, Bwana. Nisamehe, makosa yangu yote na shida. Nifanye imara na mwenye nguvu, Bwana, katika Roho wa Mungu, nipate kuwaleta watu Kwako.

213 Na bariki kusanyiko hili, kwa maana tunaomba katika Jina Lake. Samehe kila mwenye dhambi. Ongoa kila aliyerudi nyuma.

214 Wakati tumeinamisha vichwa vyetu, na kila mwanamume mwenye dhambi na mwanamke ndani hapa sasa hivi, wavulana wadogo na wasichana, ninyi nyote. Baadhi yenu vijana kule nyuma, ilinibidi kuwazungumzia kwa ukali, usiku wa juzi. Ninachukia kufanya hivyo. Mungu aibariki mioyo yenu. Huenda mlifikiri ya kwamba Ndugu Branham alikuwa mkali, lakini ni—ninawapenda. Nimeketi mahali mlipoanzia. Ninajua jinsi ilivyo; hiyo ndiyo sababu nilisema hivyo, kuona kama hamngempenda Bwana wetu. Niombeeni, ombeni kwamba huu utakuwa ndio wakati wangu wa kujiweka wakfu. Baadhi yenu ninyi mama na baba, wazee, ufanyeni huu kuwa ni wakati wa kujiweka wakfu, hivi sasa, sivyo? Mkubali moyoni mwako. Mwamini kwa nafsi yako yote.

215 Sasa wakati vichwa vyetu vimeinamishwa, kuna mtu angetaka kukumbukwa katika maombi? Kama ungetaka, inua tu mkono wako, useme, "Ndugu Branham, nikumbuke. Ninataka kuwa karibu zaidi na Mungu." Vema, dazani za mikono.

216 Baba, wakumbuke wote. Ninaomba utatutajalia; watakuwa na amani. Wakati machozi yanatiririka mashavuni mwetu na kudondoka kutoka hapa, pamoja na yangu, mimbara. Baadhi yao wakiwa na leso. Baadhi yao, watu wakubwa, wenye maungo manene, wagumu hapa ndani, walioketi hapa mbele yangu, machozi yakitiririka nyusoni mwao na mashavu yenye makunyanzi. Tupokee, Bwana. Msamehe kila mmoja wetu aliye kwenye Uwepo huu wa Kiungu. Mungu mpendwa, usiku wa leo, tusamehe, Bwana, vijana kwa wazee. Jalia tuokolewe kwenye

Siku hiyo, na tupelekwe kwenye Ufalme Wako, kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

217 Sasa mnaweza kusimama kwa miguu yenu, polepole. Sasa endeleeni kuinamisha vichwa vyenu. Polepole:

> Karibu na Wewe, Mungu wangu;
> Karibu zaidi, Bwana wangu;
> Siku zote niwe . . .

218 [Ndugu Branham anawaombea watu polepole—Mh.] "Mungu, Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Njoo, Bwana, bariki mioyo hii. [Ndugu Branham anaendelea kuomba pamoja na watu.]

219 Tafadhalini mninii tu, kwa uchaji, bila kuzungumza na mtu ye yote, hata kidogo, bila kusema neno moja zaidi, ondokeni tu kwenye jengo, kimyakimya sasa, na mwende manyumbani kwenu. Geukeni tu mwende makwenu sasa. Bila kusema neno, geukeni mtoke nje. Mungu awe pamoja nanyi.

220 [Ndugu Branham anatulia wakati kusanyiko linapoanza kuondoka kimyakimya jengoni, wakati mpiga kinanda na mpiga piano wanaendelea kucheza *Karibu na Wewe, Mungu Wangu*—Mh.]

221 "Sisi sote kama kondoo tumepotea; Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote. Lakini alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake." . . .? . . . "Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, amepigwa, na kuteswa."

222 [Ndugu Branham anaendelea kuwaombea watu kimoyomoyo, wakati mpiga kinanda na mpiga piano wanaendelea kucheza *Karibu na Wewe, Mungu Wangu*—Mh.]

Ukatili wa Dhambi, Na Adhabu Iliyogharimu Kuondoa Dhambi Maishani Mwetu SWA53-0403
(The Cruelty Of Sin, And The Penalty That It Cost To Rid Sin From Our Lives)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, 03 Aprili, 1953, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2003 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2003 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org